

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI,**  
**SHULE YA SEKONDARI ILONGO, SLP 412, MAFINGA.**  
**TAREHE 11/12/2020**

JINA LA MWANAFUNZI. ....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA**  
**SHULE YA SEKONDARI ILONGO, WILAYA YA MUFINDI, MKOA WA**  
**IRINGA MWAKA 2021.**

**UTANGULIZI:-**

Ninapenda kutumia fulsa hii kukupa taarifa kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ILONGO kwa mwaka 2021 .Shule ipo katika Kijiji cha Ugenza Kata ya Ikweha, Taarafa ya Sadani, wilaya ya Mufindi.

Hali ya hewa ni nzuri kwa masomo, shule hii ni ya kutwa na ni mchanganyiko wa wavulana na wasichana. Shule hii inafundisha masomo yafuatayo;

**Hisabati, Jiografia, Historia, Uraia, Biolojia, Kiswahili, Kiingereza, Fizikia na Kemia.**

**KUFUNGUA SHULE:-**

Shule itafungua tarehe **11/01/2021**, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** ukiwa na mahitaji yote uliyoagizwa hapo chini, kumbuka masomo yataanza Siku ya kufungua shule yaani tarehe **11/01/2021**.

**VIFAA VYA TAALUMA:**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo:-

- i. Daftari 10 counter book
- ii. Bunda moja ya karatasi (Ream) kwaajili ya mitihani.
- iii. Kalamu ya mkaa (pencil)
- iv. Kalamu ya wino
- v. Rula
- vi. Mfuko wa kubebea Daftari (BEGI)
- vii. Dictionary 1 (English to English)
- viii. Mkebe mmoja.
- ix. faili moja kwa ajili kutunzia kumbukumbu zake

## **SARE YA SHULE**

### **WAVULANA**

1. Suruali mbili zote rangi ya kijani mgomba.
2. Shati nyeupe mbili, moja mikono mifupi na nyingine mikono mirefu.
3. Viatu vya ngozi vya kamba jozi 2 rangi nyeusi. (boot haziruhusiwi kabisa)
4. Soksi jozi 2 rangi nyeusi.
5. Sweta mbili zote rangi ya kijani mgomba.
6. Tai 2 zote rangi ya kijani mgomba.

### **WASICHANA**

1. Sketi mbili zote rangi ya kijani mgomba (Rinda Box)
2. Shati nyeupe 2, moja mikono mirefu na nyingine mikono mifupi
3. Viatu vya ngozi vya kamba jozi 2 rangi nyeusi. (boot haziruhusiwi kabisa)
4. Soksi jozi 2 rangi nyeupe
5. Sweta mbili zote rangi ya kijani mgomba.
6. Tai 2 zote kijani mgomba.

**NB:** kila mwanafunzi ashone sare kwa kuzingatia rangi na aina ya kitambaa alichoelekezwa na zenye maadili.

### **SARE ZA MICHEZO**

- i. Tracksuit jozi moja rangi ya nyeusi
- ii. Tshirt ya njano moja au zaidi
- iii. Raba /viatu vya michezo

### **SHERIA NA KANUNI ZA SHULE:**

Shule in aendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu sayansi na Teknolojia na Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye usimamizi wa uendeshaji wa Elimu. unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo kipindi chote cha uanafunzi wako.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, na wanafunzi wenzio
2. Mahudhurio mazuri kila siku kwa kuzingatia ratiba ya shule
3. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
4. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wowote wa uanafunzi wako katika shule hii.
5. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
6. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
7. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
8. Kutunza mali za umma

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI**  
**KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

- i. Wizi
- ii. Uasherati
- iii. Ubakaji
- iv. Ulevi wa pombe, uvutaji bangi na madawa ya kulevya
- v. Kupiga au kupigana
- vi. Makosa ya jinai
- vii. Kudharau au kuharibu bendera ya Taifa
- viii. Kupata mimba au kusababisha mimba
- ix. Kutoa mimba
- x. Kukataa adhabu kwa makusudi/kiburi.
- xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- xii. Kuwa na simu ya mkononi
- xiii. Kuoja au kuolewa
- xiv. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

**MAMBO MENGINE MUHIMU YANAPASWA KUKAMILISHWA NA**  
**KUWASILISHWA SHULENI ANAPORIPOTI MWANAFUNZI**

Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.

Fomu ya tamko la mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

**KARIBU SANA ILONGO SEKONDARI**

.....  
**PASTORY .N. HAONGA**  
**MKUU WA SHULE**